# HIFADHI YA TAIFA
# MTO UGALLA

*Kiswahili*





## *Karibu Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla!*


**Hii ni moja kati ya hifadhi kubwa na ya kipekee ambayo bado haijatembelewa iliyo na aina nyingi za wanyama na mimea jambo linaloifanya hifadhi hii kuwa eneo mahususi kwa ajili ya utalii. Kuwepo kwa mto ugalla wenye kingo pana zilizopambwa na maji yanayotiririka kwa taratibu, wenye madimbwi, maziwa madogo madogo na maeneo oevu yenye mikunjo maridadi inayotoa makazi kwa Ndege kama Korongo nyangumi, Fundi chuma, korongo marabu, korongo domo wazi, Korongo kisiwa, Bata bukini, Tetere macho meusi, Yange yange n.k**

**Hifadhi hii imetunza mazingira yake ya asili ya nyika yaliyo ya kipekee jambo ambalo linaifanya hifadhi hii kuwa chaguo la wageni kuja kutembelea pindi wanapokuja kutembea hifadhi za mzunguko wa Magharibi**

**Hifadhi ina watumishi rafiki, wenye weledi wa kutosha, wenye kujali wateja na walio tayari kukuhudumia na kuhakikisha safari yako inakuwa ya kipekee kabisa unapokuja kutembelea hifadhi hii.**

# Historia ya Hifadhi

Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla ilianzishwa rasmi tarehe 29.11.2019 kwa tangazo la Serikali Na. 936 la tarehe 29.11.2019 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 3,865. Hifadhi hii ilipatikana kwa kuunganisha sehemu mbili zilizokuwa za mapori ya akiba yaani Pori la Hifadhi ya Msitu la Ugalla Kaskazini (kilomita za mraba 2054) pamoja na sehemu ya pori la Akiba la Ugalla (Ugalla Game




Reserve) kwa upande wa Kaskazini-Magharibi (Kilomita za mraba 1,811) na hivyo kufanya jumla ya kilomita za mraba 3,865".

Jina la Hifadhi limetokana na Mto Ugalla ambao ni chanzo pekee cha maji kwa Wanyama kipindi cha kiangazi. Mto huu hutiririsha maji yake kupitia ardhi oevu iliyopo nje ya Hifadhi inayoungana na mito mingi inayounda eneo la ardhi oevu la Moyowosi ambapo maji haya hutiririka hadi Ziwa Tanganyika

Miaka ya 1920 kulitokea Mbung'o wengi sana maeneo ya porini na maeneo yanayoitwa Ikunkwa kwa leo. Mbung'o hao walidhuru na hata kuua watu. Hivyo Serikali ya mkoloni (Waingereza) waliwaondoa wananchi na kuwa hamishia vijiji vya Uyumbu, Uruira na Kaliua kutokana na kuzuka ugonjwa wa Malale katika eneo hilo.

Wazungu hao waliwakuta wazawa wa huko wamevaa Manyoya



meupe kichwani ambayo waliyatumia kwa ajili ya matambiko. Manyoya hayo yalijulikana kwa lugha ya wenyeji kama "Ngalla". Wazungu hao walipouliza hicho mumeva nini, Wazawa (Wanyamwezi na Wakibende) wa huko maporini wakasema ni "Ngalla". Hapo wazungu hao wakasikia kama "Ugalla". Basi ndipo neno Ugalla likazaliwa na kutumika mpaka leo.

## Jinsi ya Kufika Hifadhini

**Kwa njia ya Barabara:** Kwa kipindi cha kiangazi kuanzia mwezi Juni hadi Novemba, hifadhi inafikika kwa njia ya barabara kutoka mji wa Tabora (km 170), toka





Wilaya ya Kaliua (45km) na kutoka Wilaya ya Urambo (km 75).

**Kwa njia ya anga:** Kwa kutumia ndege za kukodi, hifadhi inafikika kupitia viwanja vya ndege vilivyo karibu vya Tabora, Urambo na Kaliua. Pia wageni wanaweza kutumia viwanja wa ndege vilivyopo hifadhini vya Muhuba, Siri na Kasense ambapo viwanja hivi vinatumika kipindi cha kiangazi tu.

**Kwa njia ya treni:** Kwa kutumia treni, hifadhi inafikika kwa kupitia njia ya Kigoma – Tabora na kushuka kwenye kituo cha Usoke na Kaliua au njia ya Mpanda – Kaliua na kushuka kituo cha Lumbe na Ugalla.

## Hali ya Hewa



Hali ya hewa ya hifadhi ni ya kitropiki ambapo msimu wa mvua ni kuanzia mwezi Novemba hadi Mei ambapo msimu wa mvua nyingi ni kati ya mwezi Aprili hadi Mei. Wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya Milimita 800 hadi 1000 wakati hali ya joto kwa nyakati za kiangazi ni kati ya nyuzijoto za sentigredi 28 hadi

30 na kwa kipindi cha mvua ni kati ya nyuzijoto za sentigredi 15 hadi 21.

# Vivutio.

- **Viumbe pori**

  Hifadhi hii ina aina nyingi za wanyama kama vile tembo, Palahala, Simba, Nyamera, Korongo, Swala pala, Mbwa mwitu, Tandala mkubwa, Kongoni, Chui, Nyati, Mamba, Nsya, Pofu, Fisi, Bweha, Taya, Tohe, Pundamilia na Nzohe ambao wanapatikana zaidi maeneo oevu ya Magharibi mwa hifadhi.

- **Uoto wa asili**

  Hifadhi imepambwa na aina mbili za uoto wa asili ambapo uoto wa kwanza ni ule wa miombo na wa pili ni uoto wa Zambezi wenye maeneo ya nyasi zenye maji mengi. Uoto huu wa Miombo umegawanyika katika uoto wa nyasi wenye miti ya miombo, uoto wa miombo ulio juu ya vilima na ule ulio na maeneo oevu na nyasi ambao ndio umechukua eneo kubwa la hifadhi. Aina hii ya uoto unaifanya hifadhi kuwa ya kipekee kwa wageni kufanya utalii wa kupiga kambi ya kupumzikia huku ukiwa unaagalia wanyama walioenea kila kona.

- **Mandhari ya Mto Ugalla**

  Mwonekano mzuri wa mikunjo ya mto Ugalla, mabonde na nyika kubwa zilizopambwa na vilima vinaipa hifadhi mwonekano wa kipekee na unaovutia

- **Vichuguu vya mchwa**

  Uwepo wa vichuguu vya michwa vinavyojitokeza kwenye ardhi ya tambarare vinatoa mazingira mazuri kwa wanyama wawindao ambao husimama juu yake na kuangalia mawindo yao kwa urahisi.



- **Mto Ugalla**

  Mto huu unapita katikati ya hifadhi ndio kivutio kikuu ambapo unatoa mazingira mazuri kwa wanyama wa aina mbalimbali ambapo unatoa fursa nzuri kwa watalii kuona wanyama hawa kwa urahisi. Mto huu ndio uhai wa hifadhi hii kwani unatoa makazi kwa wanyama wa ardhini na wale wanaoishi kwenye maji na ndio chanzo kikuu cha maji kwa kipindi cha kiangazi.

- **Mamba wakubwa**

  Hifadhi hii ina mamba wakubwa ambapo katika historia ndio eneo pekee lenye mamba wakubwa zaidi Afrika ambao ni jamii ya wanyama wakubwa waliokwisha toweka duniani – dinosauri. Kwa kipindi cha mvua mamba hawa



wanakula zaidi samaki na kwa kipindi cha kiangazi huwa wanawinda wanyama ili kujitosheleza kwa chakula.



- **Maeneo ya Kihistoria**

Kuwepo kwa maeneo ya Kihistoria ya Mfinula iliyopo Ikunkwa, Senga II na Ilyamchele kunatunza historia na tamaduni ya wakazi walioshi maeneo haya.

## Aina za Utalii (Mazao ya Utalii)

- **Utalii wa kutembea kwa miguu**

Utalii huu hufanyika maeneo maalum na watalii husindikizwa na askari wa hifadhi. Utalii huu hutoa nafasi ya kuona mazingira ya asili kwa karibu na hivyo kuongeza furaha kwa watalii.

Utalii huu unaweza fanyika kwa muda mfupi hadi masaa manne na muda mrefu kuanzia masaa 4 na kuendelea kutegemea na matakwa ya mteja

- **Utalii wa mbuga na kuvinjari nyikani**

Watalii wengi hupenda kutembelea mbuga na kuvinjari nyikani ili kujionea mandhari, wanyama, ndege, na wadudu mbalimbali. Utalii huu hutumia magari madogo na makubwa kama





- **Kuangalia ndege**

  Utalii huu humwezesha mtalii kuona aina mbali mbali za ndege wanao patikana Hifadhini, anaweza kuona ndege hao kwa kuangalia kwa macho au kifaa maalumu "Binocular". Hifadhi ina ndege Zaidi ya 147.

- Utalii wa kupiga picha

  Huu ni utalii wa kutazama mandhari na kupiga picha. Upigaji picha wa kawaida unaruhusiwa ila upigaji picha wa biashara unahitaji vibali maalum ikiwa ni pamoja na kulipiwa.

- **Utalii wa kula chakula porini**

  Utalii huu unamwezesha mgeni kula chakula porini huku akifurahia mandhari ya asili. Utalii huu hufanyika baada ya kulipia tozo

- **Utalii wa kutazama jua la machweo**

  Utalii huu unamwezesha mgeni kukaa porini na kutazama jua linapo zama majira ya jioni na kufurahia mandhari nzuri

# Malazi.

Hifadhi inatoa malazi kwenye kambi za jumuiya na kambi maalumu ambapo mgeni anatakiwa kuja na hema na vitu vingine vitakavyo muwezesha kulala na kula. Taarifa za awali zinahitajika kabla ya kupanga safari ya kuja kulala hifadhini.

# GHARAMA ZA KUTEMBELEA HIFADHI

| | *Waafrika Mashariki Tshs* | *Wasio wa Afrika Mashariki US $* | *Wasio wa Afrika Mashariki waishio Tanzania US $* |
|---|---|---|---|
| **A. Tozo ya Uhifadhi kwa mtu kwa siku** | | | |
| i. Umri wa miaka 16 na zaidi | 4,000 | 20 | 20 |
| ii. Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 2,000 | 20 | 20 |
| iii. Umri chini ya miaka 5 | Bure | Bure | Bure |
| **B. Kupiga kambi - Kambi za jumuiya** | | | |
| i.Umri wa miaka 16 na zaidi | 5,000 | 30 | 30 |
| ii. Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 3,000 | 20 | 20 |
| iii. Umri chini ya miaka 5 | Bure | Bure | Bure |
| **C. Kupiga kambi - Maeneo maalum** | | | |
| i. Umri wa miaka 16 na zaidi | 10,000 | 50 | 50 |
| ii. Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 5,000 | 10 | 10 |
| iii. Umri chini ya miaka 5 | Bure | Bure | Bure |
| **D. Hotel Concession (Kwa mtu mmoja/Usiku mmoja)** | | | |
| i. Umri wa miaka 16 na zaidi | 20,000 | 25 | 25 |
| ii. Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 5,000 | 10 | 10 |
| iii. Umri chini ya miaka 5 | Bure | Bure | Bure |
| **E. Bush Meal** | 5,000 | 5 | 5 |
| **F. Utalii wa Matembezi kwa miguu** | | | |
| i. Matembezi ya muda mfupi(saa 1 hadi 4) kwa watu wazima | 5,000 | 20 | 20 |
| ii. Matembezi ya muda mfupi kwa watoto wenye umri zaidi ya miaka 12 | 2,500 | 10 | 10 |
| iii. Matembezi ya muda mrefu (zaidi ya masaa 4) kwa watu wazima | 10,000 | 25 | 25 |
| iv. Matembezi ya muda mrefu kwa watoto wenye umri zaidi ya miaka 12 | 5,000 | 15 | 15 |
| **G. Tozo ya kuongoza wageni porini wakiwa ndani ya gari au tozo ya askari kwa matembezi ya miguu (Kwa kikundi kwa safari)** | 30,000 | 40 | 40 |
| **H. Tozo za magari** | | | |
| i. Uzito hadi kilo 2000 | 20,000 | 50 | |
| ii. Uzito kilo 2,001 hadi 3,000 | 50,000 | 150 | |
| iii. Uzito kilo 3001 hadi 5,000 | 75,000 | 200 | |

| | Usajili TanzaniaTShs. | Usajili kigeni US$. |
|---|---|---|
| iv. Uzito kilo 5001 hadi 7000 | 100,000 | 300 |
| v. Uzito zaidi ya tani 10 (ruhusa toka kwa Kamishna Uhifadhi) | 125,000 | 125 |

vi. Magari ya wazi yatatozwa asilimia 50 zaidi ya tozo za kawaida

**I. Faini kwa kuzidisha mwendo**

(aina zote za magari) Tshs. 50,000/=

Faini kwa kusababisha ajali TShs. 200,000

**J Tozo ya kupiga picha za matangazo ya biashara**

Hujumuisha ada ya kuingia na kupiga kambi hifadhini bila kujali utaifa wa mpiga picha US $ 200 kwa mtu kwa siku

**K "Video Shooting"**

Kwa kikundi cha watu kuanzia 2 hadi 20 Sh.100,000 kwa Watanzania na $ 100 kwa Wasio Watanzania/wakazi

**L Tozo kwa makundi ya wanafunzi au binafsi**

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. Tozo ya Uhifadhi kwa shule za msingi, sekondarina kidato cha 5&6 | 2,000 | 10 | 10 |
| ii. Tozo ya uhifadhi kwa vyuo na vyuo vikuu | 5,000 | 10 | 10 |
| iii. Tozo ya kupiga kambi kwa shule za msingi, sekondari na kidato cha 5&6 | 2,000 | | |
| iv. Tozo ya kupiga kambi kwa vyuo na vyuo vikuu | 3,000 | | |
| v. Malazi ya nyumba na hosteli kwa wanafunzi | 5,000 | | |

**M Tozo Kutua ndege**

| | **Ndege zilizosajiliwa TZ zenye ratiba maalumu** *(kwa mzunguko ndani ya Hifadhi moja)* **Tshs** | **Ndege za kukodi zilizosajiliwa Tanzania** *(kwa mtuo mmoja)* **(TShs)** | **Ndege zilizosajiliwa nje ya Tanzania** *(kwa mtuo mmoja)* **US$.** |
|---|---|---|---|
| a) Kiti 1 hadi 4 | 50,000 | 40,000 | 100 |
| b) Viti 5 hadi 12 | 60,000 | 50,000 | 150 |
| c) Viti 13 na kuendelea | 80,000 | 70,000 | 300 |

**N Tozo kwa (magari yasiyo ya kibiashara, tela,boti, na ndege) ambazo zimesajiliwa Tanzania na zinazokaa ndani ya Hifadhi kwa mwaka.**

i. Uzito hadi kilo 2000 50,000

| | | |
|---|---|---|
| ii. | Uzito kuanzia kilo 2,001hadi 3,000 | 100,000 |
| iii. | Uzito kuanzia kilo 3,001 hadi 7,000 | 200,000 |
| iv. | Uzito kuanzia kilo 7001 hadi 10,000 | 50,000 |
| v. | Trekta, Tela na Boti | 50,000 |
| v. | Ndege | 200,000 |

**O Tozo ya uwanja wa ndege inalipwa kwa mtu mmoja anapotua ndani ya hifadhi na kwenda kulala nje ya Hifadhi**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Raia wa Afrika mashariki | TShs 10,000 |
| ii. | Raia wasio wa Afrika mashariki, na wageni wakaazi wanaoishi Tanzania | US $ 10 |

**P Pasi ya Mkurugenzi kwa mwaka US $ 100**

(Yahitaji ruhusa toka kwa Kamishna wa Uhifadhi)

**Q Kuingia na kutoka zaidi ya mara moja Hifadhini**

Kuingia na kutoka zaidi ya mara moja Hifadhini itategemea na aina ya kibali cha kuingia hifadhini

i. Kibali cha safari ya kutwa, ambacho kinadumu hadi saa kumi na mbili jioni, kitaruhusu mgeni kutoka na kuingia zaidi ya mara moja ndani ya muda huo

ii. Kibali cha safari ya kulala, ambacho kinadumu kwa masaa ishirini na nne, kitaruhusu mgeni kutoka na kuingia zaidi ya mara moja ndani ya muda huo.

**Zingatia:**

- Mwenye kibali maalumu cha Mkurugenzi Mkuu,hapaswi kuambatana na wageniwengine
- Tozo zikilipwa hazirudishwi
- Malipo yote hufanyika kwa kadi za kielekroniki (visa, master card), mitandao ya simu katika malango ya kuingilia hifadhini.
- Tozo za kiingilio na Magari zitaweza kutumia kuingia Hifadhini zaidi ya mara moja ndani ya masala 12 au 24
- Tozo zote hapo juu hazijajumuishwa na ongezeko la kodi (VAT 18%)

# Tembelea Hifadhi

*Tafadhali tembelea hifadhi hii ili ujionee upande mwingine wa uasili pale utakapokutana na tamaduni za wazawa na pia waweza kusaidia hifadhi ili kuwawezesha kiuchumi. Karibu!*

# Kanuni na Taratibu za Hifadhi

- Hairuhusiwi kuua, kusumbua au kulisha  wanyama hifadhini
- Hairuhusiwi kupiga kelele kama honi za magari, muziki kwa sauti kubwa au usumbufu mwingine wowote kwa wageni wengine
- Acha mimea yote wanyama, mafuvu, mifupa, miamba unapovikuta
- Ni marufuku kutupa taka hifadhini
- Usiwashe moto kwenye hifadhi isipokua kwenye kambi zinazoruhusiwa
- Hairuhusiwi kuingia na wanyama wafugwao hifadhini
- Hakikisha hauendeshi zaidi ya mwendokasi wa km50/saa kwa ajili ya usalama wako na Wanyama
- Hairuhusiwi kuendesha nje ya barabara isipokuwa mahali ambapo utakua umeruhusiwa
- Hairuhusiwi kuingia na bunduki au silaha ya aina yeyote ndani ya Hifadhi

**Kumbuka**

- Kuwa ndani ya hifadhi kabla ya saa 12:00 asubuhi na baada ya saa 12:00 jioni ni kosa, isipo kuwa kwenye maeneo ya kulala wageni yanayotambulika.





**Kwa mawasiliano zaidi**

**Mkuu wa Hifadhi,**

Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla,

S. L. P 08 Kaliua,Tabora-Tanzania

**Simu:** +255 747 980 639/ +255 762 324 999/ +255 754 469 865

**Baruapepe:** ugalla@tanzaniaparks.go.tz

**Tovuti:** www.tanzaniaparks.go.tz

**Instagram:** ugalla_river_nationalpark

*Tafadhali pakua kipeperushi chetu*